# HALMASHAURI YA WILAYA YA KILINDI

**SHULE YA SEKONDARI LWANDE**

S.L.P 53, SONGE – KILINDI

**SIMU: 0625378675 /**

TAREHE: 11.12.2020

**JINA LA MWANAFUNZI:** ____________________________________

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LWADE**

**KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021**

Ninayofuraha kukufahamisha kuwa, umechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Lwande kidato cha kwanza mwaka 2021.

Shule itafunguliwa tarehe 11.01.2021 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe 11.01.2021.

**1. MAMBO YA MUHIMU YA KUFANYA**

Kusoma kwa makini maelezo yote yaliyopo kwenye fomu hii ya kujiunga ( joining instruction) ya shule hii na kutekeleza bila kisingizio maelekezo yote ili kuleta ufanisi wenye tija katika kukupatia elimu iliyo bora kwa muda wote wa masomo.

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### SARE ZA SHULE

**Maelekezo kuhusu mshono na aina ya kitambaa yanapatikana shuleni.**

#### A. WAVULANA

i. Shati jeupe la mikono mifupi

ii. Suruali ya kijani ndefu

iii. Sweta la rangi ya blue

#### B. WASICHANA

i. Sketi rangi ya kijani

ii. Shati jeupe la mikono mifupi

iii. Sweta la rangi ya blue

- **Mzazi anatakiwa amnunulie mwanafunzi viatu vyeusi visivyo na kisigino kirefu vya kufunga na kamba pamoja na soksi nyeupe ndefu kwa Wasichana na soksi nyeusi ndefu kwa Wavulana.**

## 3. MAHITAJI YA DARASANI

i. Mwanafunzi anapaswa kuwa na makubwa (counter book ) madaftari 12
ii. Kalamu za risasi za kutosha na vifutio na rula
iii. Kalamu za kutosha za wino wa bluu au nyeusi

## 4. VIFAA ANAVYOTAKIWA KUJA NAVYO MWANAFUNZI

i. Fyekeo 1
ii. Jembe 1
iii. Ndoo ndogo ya 1 lita 10
iv. Fagio la chelewa 1

## 5. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

i. Kuwepo ndani ya mipaka ya shule muda wote wa masomo na kazi
ii. Kuhudhuria vipindi vyote vya shule darasani na nje ya darasa
iii. Ifahamike kuwa kutoroka vipindi au shuleni ni kosa kubwa
iv. Kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote wakiwemo walimu wanapoingia darasani na maeneo mengine wakubwa watakapokuwepo

v. Kutotimia lugha mbaya wakati wote kati yako na wanafunzi wengine au kwa walimu na kwa watu wengine

vi. Kutovaa vidani kama vile herein, mikufu , bangili , kutotia dawa nywele

vii. Kutojichora kwa hina au tattoo sehemu za mwili wako

viii. Ni lazima kusimama mwalimu aingiapo darasani na kusalimia

ix. Kutotembelea nyumba za kulala wageni na kumbi za starehe

x. Kutokuwa na kucha ndefu na kutopaka rangi au hina

xi. Kuheshimu wafanya kazi wote waliopo shuleni kama walezi wao

xii. Wavulana hawaruhusiwi kufuga ndevu wala nywele ndefu

xiii. Nywele zikate nusu inch

xiv. Lugha chafu na matusi ni marufuku

xv. Kuvaa sare za shule wakati za masomo darasani nje ya shule kwa shughuli za kishule , anapokwenda hospitali na maeneo mengine

xvi. Kutokuwa na simu ya mkononi

xvii. Kutovaa kofia, jaketi na sweta ambazo sio za shule

xviii. Kufanya usafi binafsi na wa shule, mazingira na madarasa

xix. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote

xx. Kutokwenda nyumba za walimu au wafanyakazi wengine bila ruhusa maalum

xxi. Mafuta yenye harufu kali hayaruhusiwi

xxii. Kuheshimu bendera na wimbo wa taifa

*NB: Adhabu kali zitatolewa kwa wanafunzi wote watakaokiuka sheria za shule , simu , nguo za nyumbani na vitu vingine visivyotakiwa shuleni*

*vitachukuliwa na havitarudishwa.*

**MAKOSA YAFUATAYO YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi

ii. Uasherati , ubakaji , ushoga na ulawiti

i. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya , biashara ya madawa yeyote ya kulevya
ii. Makosa ya jinai
iii. Kupigana au kupiga mwanafunzi mwenzake, mwalimu au mtumishi asiye mwalimu
iv. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine
v. Kudharau bendera na wimbo wa taifa
vi. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
vii. Kutoa au kushawishi kutoa mimba
viii. Kuoa au kuolewa
ix. Kugoma , kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni
x. Kukataa adhabu iliyotolewa na mwalimu
xi. Utoro(kukaa nje ya shule bila taarifa kwa zaidi ya siku 90)
xii. Kukataa kufanya mazoezi na mitihani shuleni
xiii. Kuwa na simu ya mkononi
xiv. Kutembelea nyumba za kulala wageni, kumbi za starehe, baa , klabu, na sehemu zingine ambazo kisheria mwanafunzi haruhusiwi

**MWISHO**

Nachukua nafasi hii kukukaribisha shule ya sekondari Lwande na ni matarajio yangu kuwa utaitumia vyema nafasi hii uliyopewa na Taifa lako.

..............................

PETER H MAINA

***Mkuu wa Shule***

Lwande Sekondari

HEADMASTER LWANDE SEC. SCHOOL KILINDI

**TAARIFA YA MZAZI / MLEZI**

Mimi ………………………………………. Mwenye simu namba ……………………. Ninakubali kwa hiari yangu mwanangu asome katika Shule ya Sekondari Nkama kuanzia tarehe 06.01.2020

Na ninaahidi kama ifuatavyo: -

i. Kumpatia mwanangu vifaa vyote kama vilivyoainishwa katika fomu ya kujiunga ikiwemo sare kamili ya shule
ii. Ninatambua ya kuwa walimu wanahitaji ushirikiano wangu katika kumpatia mwanangu elimu na nitashirikiana nao bega kwa bega kwa masuala yanayomhusu mwanangu Kitaaluma na Kinidhamu ili aweze kufikia malengo yake ya Taifa
iii. Naahidi kuwa endapo mwanangu ataenda kinyume na taratibu zilizoanishwa katika fomu hii achuliwe hatua stahili za kinidhamu